**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo

*Jemima Lenjima[1*] na Dkt Julius Edmund Frank, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, S. L. P. 23409, Dar es Salaam, Tanzania.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0009-009-5050-1739; Barua pepe ya mawasiliano: lenijmajemima7@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1396**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*28 Agosti 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Jina, Majina ya Asili, Jamii-lugha, Wagogo.*

**IKISIRI**

Miaka ya hivi karibuni majina ya asili katika jamii nyingi za kitanzania yamekuwa yakikabiliwa na changamoto ya kupotea kwa kasi hasa kwa vijana kutokana na ujio wa sayansi na teknolojia pamoja na dini. Makala haya yamekusanya na kubainisha majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo. Makala yameongozwa na swali moja katika kuandaliwa kwake. Swali hilo linauliza; Majina yapi ya asili ya watu yanayotumika katika jamii-lugha ya Wagogo? Mbali na kujadili swali hilo muhimu, Makala haya pia yametoa mapendekezo kuhusu njia za kuendeleza matumizi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha husika. Data za makala zimekusanywa kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali kwa ufafanuzi zaidi. Uchanganuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Uumbaji ya (Sapir-Whorf, 1958) inayosisitiza kwamba, lugha ndio msingi wa kuuelewa ulimwengu. Unapojifunza lugha hiyo hata dunia unayoiumba akilini mwako itatokana na dunia iliyoratibiwa na wasemaji wake. Matokeo ya uchunguzi wa makala haya yamedhihiridha kuwa, majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yapo katika makundi kulingana na jinsi yanavyotolewa au kupatikana. Makundi yamebainishwa kwa kuzingatia sifa zinazofanana katika makundi mbalimbali.

**APA CITATION**

Lenjima, J., & Frank, J. E. (2023). Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 303-318. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1396.

**CHICAGO CITATION**

Lenjima, Jemima and Julius Edmund Frank. 2023. “Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo”. *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 303-318. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1396.

**HARVARD CITATION**

Lenjima, J., & Frank, J. E. (2023) “Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo”, *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 303-318. doi: 10.37284/jammk.6.1.1396.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1396

**IEEE CITATION**

J., Lenjima, & J. E., Frank "Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 303-318, Aug. 2023.

**MLA CITATION**

Lenjima, Jemima & Julius Edmund Frank. "Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo ". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Aug. 2023, pp. 303-318, doi:10.37284/jammk.6.1.1396.

## UTANGULIZI

Dhana ya majina na maana zake ni kongwe sana na yenye uhai hata sasa katika tamaduni nyingi ulimwenguni. Majina ndiyo yanayomtambulisha mtu, kitu na mahali katika jamii zote ulimwenguni. Utoaji wa majina ya watu katika jamii nyingi za Kiafrika haufanyiki kiholela bali huzingatia vigezo, taratibu na kanuni fulani zilizobeba maana kulingana na mila na desturi za jamii hiyo. Utambulisho huo unatofautiana kwa maumbo, muundo na uwasilishaji mbalimbali kwa utambulisho husika. Makala haya yameainisha majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo. Kama ilivyo katika jamii-lugha nyingine ulimwenguni, Wagogo wanatambulisha watu wake kwa kuwapa majina. Matsimela (1997) alisema kuwa, huko nyuma katika jamii nyingi za Kiafrika, mtoto alipozaliwa alipewa jina kwa kufuata kanuni na taratibu fulani zinazotofautiana toka kabila moja na jingine kulingana na mila na desturi za watu wa jamii alipozaliwa mtoto huyo. Hii ni kwa sababu jina la jamii fulani hufungamana na imani fulani ambayo huambatana na mila na desturi za utamaduni wa jamii husika. Mbiti (1990) alisema kuwa katika imani za Kiafrika, majina yana athari katika tabia ya mtoto, afya ya mtoto, mafanikio ya mtoto na hata maendeleo ya mtoto ya baadaye. Mawazo ya Mbiti yaliungwa mkono na Koigi (2008); Rugemalira (2005); Matsimela (1997) na Rey (1995) ambapo walisema kuwa, jina husaidia katika utambuzi wa mtu binafsi, kijamii, kiutamaduni na hata kiuchumi. Pia, jina hilohilo humtambulisha mtu eneo analotoka, huashiria tabia yake, sifa zake, imani na fikra zake. Hata hivyo, hivi sasa utamaduni huu wa kuita watoto majina ya asili, ambao ulitunza asili ya watu umetoweka kwa kiasi kikubwa katika jamii-lugha ya Wagogo kwani watoto wengi wamekuwa wakipewa majina yasiyo ya asili kutokana na ujio wa vitu anuai na majina ya asili yakiachwa na kupuuzwa kabisa. Rugemalira (2005) katika utafiti wake alisema kuwa, majina na lugha nyingi za Kibantu zinafifia na hata kuwa hatarini kupotea au kutoweka kutokana na watu hasa vijana kutojua thamani iliyobebwa na majina ya lugha hizo katika utambulisho wao katika nyanja mbalimbali. Hivyo basi makala haya yameshughulika na uainishaji wa majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo kwa kuzingatia makundi mbalimbali kama yalivyojitokeza kati data uwandani.

### Historia ya Jamii-lugha ya Wagogo na Shughuli za Kiuchumi

Wagogo ni jamii mojawapo kati ya jamii nyingi zinazopatikana katika nchi ya Tanzania. Wanaishi katika mkoa wa Dodoma ambapo kwa sasa ndiyo makao makuu ya nchi ya Tanzania. Kimila, Wagogo walitambuliwa kwa kutoga *ndewe* na *malomwa* kwenye masikio na kutia *nyhende* (pengo) kwa kung'oa meno ya chini na kuchoma *nindi* katika paji la uso (Mnyampala, 1954, uk. 92). Wagogo hujishughulisha na shughuli za kiuchumi, kisiasa, kitaaluma na kiutamaduni. Kama ilivyo katika jamii-lugha nyingine ulimwenguni, Wagogo wanatambulisha watu wake kwa kuwapa majina ambayo hutolewa kwa utaratibu maalumu na sio kiholela kwa kutumia vigezo mbalimbali katika utoaji wa majina kwa jamii husika.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii imeshughulikia mapitio ya maandiko. Katika kipengele hiki maandiko mbalimbali yamepitiwa yanayohusiana na mada ya makala haya. Maeneo yaliyopitiwa ni tafiti tangulizi zilizobainisha majina ya asili ya watu katika Afrika na Tanzania.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

### Tafiti Tangulizi Zilizobainisha Majina ya Asili Katika Afrika

Musere (2010) alifanya utafiti wa majina ya watu ya jamii ya Buganda nchini Uganda. Katika utafiti wake alibaini kwamba majina ya watu yaliyo mengi katika jamii ya Buganda yanasababishwa na methali. Anaendelea kuelezea kuwa jina hilo linakuwa na heshima fulani ndani yake kwa kigezo cha kiakili, urafiki, ushirikiano, shukrani, utoaji ujinga, kusifu n.k. Katika kushadadia hoja yake Musere (keshatajwa) alitoa majina yatokanayo na methali kama vile "Ebigambo tebyasa (tibyasa) mutwe" yaani maneno hayapasui kichwa. Kutokana na methali hiyo utakuta mtoto anaitwa Tebyasa.

Dawling (2004), kwa upande wake katika kipengele cha majina ya watu anaeleza kwamba katika jamii za Kiafrika, majina huwa yanafungamana na maana mbalimbali. Anatoa mfano katika jamii ya Kizulu kwa kueleza jina kama "Lindiwe" katika jamii ile lina maana ya "kufariji" na kuwa jina hili linatolewa kwa mtu aliyekaa muda mrefu bila kuzaa lakini kwa kutarajia kwamba ipo siku atapata mtoto. Vile vile jina "Ntombizondwa" linatolewa katika familia iliyo na watoto wa kike pekee. Maelezo ya Dawling (keshatajwa) yanadhihirisha kwamba majina yanayotolewa kwa watu yana maana na dhima mbalimbali katika jamii husika. Mawazo ya Dawling yaliungwa mkono na watalaamu kama Gray (1999) na Kalkanova (1999) waliposema kuwa jina linaweza kutumika kumwakilisha mtu au jamii. Pia jina linaweza kuonesha uhusiano wa kijamii pamoja na kutunza hadhi ya jamii. Watalaamu hawa wanamalizia kwa kusema kwamba, utumiaji wa majina huwa unaendana na kanuni, sheria na desturi za jamii husika. Kwa kurejelea makala haya ni wazi kwamba majina ya asili katika jamiilugha ya Wagogo hubeba maana mbalimbali zinazotokana na mazingira ya jamii husika kwa maana, majina hayo yanapotumika huwa yanaitambulisha jamii hiyo. Ingawa makala haya hayakuchunguza utambulisho, lakini mawazo yaliyotolewa na watalaamu hawa yalikuwa msaada katika kubainisha maana za majina, historia na uzoefu wa maisha ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo.

Ota (2002) alitafiti majina ya watu ya asili katika jamii ya Edo nchini Nigeria. Katika utafiti wake anafafanua kuwa majina ya asili yamebeba dhima ya utambulisho wa dini za Afrika na kwamba mtu anaposema jina la asili huonesha ushiriki wake katika dini yake. Anaendelea kusema kuwa majina ya asili katika jamii za Kiafrika hayatolewi kiholela bali kuna kanuni mahususi zinazozingatia utamaduni wa jamii husika. Ota (keshatajwa) aliendelea kusema kuwa majina katika jamii za Kiafrika hayatolewi bila kukusudiwa au kutamkwa tu bali pia huakisi mtazamo mpana wa jamii kwani majina ya jamii ya Edo huelezea imani na fikra za jamii ya Edo. Kwa maelezo haya, Ota (keshatajwa) alisema mtazamo wa kuwa katika Afrika hakuna chochote katika majina ni kauli isiyo na mashiko katika jamii za Afrika hasa kwa utamaduni wa Edo kwani majina ya asili ya jamii ya Kiafrika ikiwemo Edo yanabeba maana maalumu tofauti kabisa na inavyotafisiriwa na wageni kutoka nje ya bara la Afrika kuwa majina ya asili ya Kiafrika hayana maana na ni majina ya kishenzi.

### Tafiti Zilizobainisha Majina ya Watu Katika Tanzania

Zacharia (2020), tafiti wake ulilenga kutathmini mitazamo ya wanajamii kuhusu matumizi ya majina ya Kiswahili jijini Dar es Salaam. Hivyo kiwango cha matumizi ya majina ya Kiswahili jijini Dar es Salaam ni asilimia 26.25 ya majina yote yaliyokusanywa katika utafiti huo. Aidha, kiwango cha matumizi ya majina kutoka lugha zingine ni asilimia 73.75 ya majina yote yaliyokusanywa katika utafiti huo. Kadhalika, asilimia 51.875 ya majina yote ya watoataarifa waliona kuwa majina ya Kiswahili yatumike katika uteuzi wa majina ya watu jijini Dar es Salaam. Ilihali asilimia 16.25 ya watoataarifa waliona kuwa majina ya kiswahili yatumike lakini majina teule yanapaswa kuwa na maana nzuri. Pia asilimia 4.375 ya watoataarifa waliona kuwa lugha yoyote inaweza kutumika katika uteuzi wa majina. Kwa upande mwingine, asilimia 23.125 ya watoa taarifa waliona kuwa majina ya Kiswahili

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

yasitumike. Hivyo, ingawa matumizi ya majina ya Kiswahili katika shughuli za kila siku jijini Dar es Salaam yaliwashawishi watoa taarifa wengi waone kuwa kuna haja ya kutumia majina ya Kiswahili lakini kuna vipengele vya kiisimu jamii kama maana za majina, kasumba za kupenda majina kutoka lugha za kigeni na athari za dini ambavyo tayari vimeukulia kiwango kidogo cha matumizi ya majina hayo.

Tegisi (2019), utafiti ulihusu uchunguzi wa kisemantiki wa majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Utafiti ulilenga kuainisha majina ya asili, kuonesha vigezo vitumikavyo katka kuteua majina ya asili na kubainisha miktadha ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa, majina ya asili katika koo za Ginantuzu yamewekwa katika makundi kumi na saba kama vile, majina yanayotokana na wanyama, vitendea kazi, mazao, vyakula, matukio, mahala pa kuzaliwa, tabia na matendo, jinsi mtoto alivyozaliwa, matunda, vitu, ukoo, mimea,itikadi za dini na utawala, ujio wa vitu vipya na unasibu. Utafiti huu pia umebaini kuwepo kwa vigezo kumi vilivyotumika katika kuteua majina katika koo za Ginantuzu. Vigezo hivyo ni kigezo cha mazingira, utani, matukio, mahusiano katika familia, urithi, tabia na matendo, uchumi wa familia, ujio wa vitu vipya, mfuatano wa watoto na itikadi za dini. Pia utafiti huu ulibaini kuwepo kwa miktadha saba ya majina ya asili katika koo za Ginantuzu ambayo ni muktadha unaodokeza ukubwa, udogo, uzuri, udunishaji, uhusiano katika familia, mazoea na tabia na matendo.

Anusa (2016), katika kutafiti maana za majina ya watu katika jamii ya Wayao alibaini kuwa watu hupewa majina katika jamii hiyo yakiwa na maana fulani. Kuna majina ambayo hutokana na tabia au sifa za mtu husika, majina yaliyotokana na matukio, mahali, wakati au misimu na majina yaliyotokana na urithi, hisia za wazazi au Imani katika jamii hiyo.

Nyangaywa (2013) alifanya utafiti kuhusu jamii ya Wajita wanaopatikana Kaskazini Magharibi mwa Tanzania (kanda ya ziwa). Katika utafiti huo alifanya uchunguzi wa kisemantiki na taratibu za utoaji wa majina ya Kijita na kubaini kuwa majina ya Kijita hayatolewi kiholela bali yanafuata taratibu mbalimbali zilizofumbata falsafa, mila na desturi za Kijita. Mtafiti pia alibaini kuwa maana za majina mengi ya Kijita zinakiliwa katika kazi, matukio, vyakula, vitoweo na usababishi wa majina ya wanyama.

## MISINGI YA NADHARIA NA METHOLODOLOJIA

Kipengele hiki kinahusiana na misingi ya Nadharia pamoja na mbinu za utafiti (metholodolojia) zilizotumika.

### Misingi ya Kinadharia

Uchambuzi wa data za makala haya umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Uumbaji ambayo iliasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani (Sapir, 1958) na kuendelezwa na (Whorf, 1958). Kimsingi, nadharia hii inaeleza kwamba, lugha ndio msingi wa kuuelewa ulimwengu. Unapojifunza lugha ni kama unatawaliwa na lugha hiyo. Hata dunia utakayoiumba akilini mwako itatokana na dunia kama ilivyoratibiwa na wasemaji wake. Watalaam hawa (wameshatajwa) wanaendelea kueleza kwamba binadamu huuona ulimwengu kupitia taratibu zilizowekwa na lugha yake ya kwanza. Ni vigumu kuchukua jina la mtu kutoka katika jamii na kumpa mtu wa jamiilugha nyingine kwa sababu jina la jamii moja hufungamana na imani hiyo ambayo huambatana na utamaduni wa jamii husika. Kutokana na maelezo hayo, watu wenye misingi tofauti ya lugha hawapati picha sawia ya ulimwengu. Ulimwengu tunamoishi kwa kiasi kikubwa umejengwa kupitia lugha za jamii fulani. Jamii zinatofautiana katika kujenga fikra na mawazo kutokana na vitu mbalimbali katika lugha husika kama ilivyo kwa majina ya asili ya watu wa jamiilugha moja na nyingine ulimwenguni, hususani barani Afrika. Sapir (1921) aliwahi kusema kuwa, wanadamu hawaishi katika ulimwengu dhahiri wala pekee bali wanazungukwa na shughuli za kijamii na kuzama katika ulimwengu wa lugha ambao ndio njia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

pekee ya kujieleza katika jamii. Lugha huakisi ulimwengu halisi kwa kiasi kikubwa na ulimwengu wa lugha umefungamana na tabia za lugha ya kundi au jamii fulani. Watu huona, husikia na huwa na tajriba ya mazingira yao kwa kuchukulia kuwa lugha zao hufafanua na kuelezea tajriba zao na hivyo, huathiri maisha yao.

Kutokana na majina ya asili tunaweza kusema kwamba jina ambalo msingi wake ni lugha linatunza historia ya jamii kwa usahihi kuliko hata maandishi ya vitabu vya historia. Hii ni kutokana na ukweli kwamba vitabu visipotunzwa vizuri huweza kupoteza historia ya jamii husika kwa kupoteza ubora wa maandishi, kuchanika au kupotea. Lakini kama, majina yataemdelea kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ni dhahiri jamii zitaendelea kutunza historia ya jamii husika kwa kupokea kutoka vizazi tangulizi. Hii inatudokeza kwamba, majina yasiyo ya jamii husika hayawezi kueleza historia ya jamii hiyo kwani majina hayo ni urithi wa jamii nyingine ambayo kwayo hutambulishwa.

## METHOLODOLOJIA

Data za makala haya imekusanywa katika mkoa wa Dodoma nchini Tanzania katika wilaya za Mpwapwa na Chamwino. Vijiji vinne vilihusishwa ambavyo ni Mima na Gulwe kutoka wilaya ya Mpwapwa pamoja na Mvumi Misheni na Handali kutoka katika wilaya ya Chamwino. Jumla ya watoataarifa arobaini na nane (48) waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji usonasibu. Data zimekusanywa kwa kutumia njia ya mahojiano na majadiliano ya Kundi lengwa, na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali kwa ufafanuzi zaidi. Nadharia ya Uumbaji ya (Sapir-Whorf, 1958) imetumika katika uchambuzi wa data.

## UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI WA DATA

Vipengele vilivyojadiliwa katika uchunguzi wa mada ya makala haya ni kukusanya na kuainisha majina ya asili ya watu miongoni mwa majina ya jamii-lugha ya Wagogo na mapendekezo kwa ujumla.

### Majina ya Asili ya Watu Katika Jamii-lugha ya Wagogo

Lengo la makala haya ni kukusanya na kuainisha majina ya asili ya watu miongoni mwa majina ya jamii-lugha ya Wagogo. Matokeo ya makala haya yamedhihirisha na kuonesha kuwa, majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yapo katika makundi kulingana na jinsi yalivyotolewa au kupatikana. Makundi yalibainishwa kwa kuzingatia sifa zinazofanana katika makundi mbalimbali. Miongoni mwa makundi hayo ni pamoja na majina ya asili ya watu yanayotokana na matukio mbalimbali, mahali pa kuzaliwa, matendo na tabia za watu, chimbuko la ukoo na majina ya asili yanayotokana na majina ya wadudu na wanyama. Majina mengine ni majina yanayotokana na utani, kipato cha familia na majina yanayotokana na urithi. Makundi hayo na majina yake ni kama yanavyowasilishwa katika sehemu ifuatayo;

### Majina ya Asili ya Watu Yanayotokana na Matukio

Matukio ni mambo yote yanayojiri katika jamii. Mambo hayo yanaweza kuiletea jamii husika furaha au huzuni. Matukio ni mojawapo ya mambo yanayoathiri majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo. Katika makala haya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yamewasilishwa na kuchanganuliwa katika makundi yafuatayo; majina yatokanayo na matukio ya vita, matukio ya majanga mbalimbali, matukio ya mahali pa kuzaliwa na matukio yanayotokana na vipindi vya misimu.

### Majina ya Asili ya Watu Yanayotokana na Matukio ya Vita

Haya ni majina ya asili ya watu ambayo hutolewa kwa wahusika kutokana na matukio tofautitofauti ya vita vilivyojitokeza katika jamii husika. Majina yatokanayo na matukio ya vita, hutolewa katika jamii-lugha ya Wagogo kwa mtoto kama jina la kurithi kutoka kwa wazazi au ndugu wa karibu kama ukumbusho. Japokuwa majina hayo kwa sasa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

hayatumiki kiukamilifu kutokana na ujio wa sayansi na teknolojia pamoja na dini. Baadhi ya majina na mifano ya majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya vita imefafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 1*.

**Jedwali 1: Majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya vita**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Dondo* | Me | Alizaliwa wakati wa ugomvi. |
| 2 | *Ilugu* | Ke | Alizaliwa wakati wa vita. |
| 3 | *Ligoha* | Me | Alizaliwa wakati wa vita. |
| 4 | *Maleo* | Me | Alizaliwa wakati wa vita. |
| 5 | *Malugu* | Me | Alizaliwa wakati wa vita. |
| 6 | *Msuliche* | Me | Alizaliwa wakati wazazi wamechukizana. |
| 7 | *Mtaze* | Ke | Alizaliwa wakati kuna ugomvi wakiomba msaada. |
| 8 | *Ndugai* | Me | Alizaliwa wakati wa vita. |
| 9 | *Nhizwa* | Me | Alizaliwa wakati baba wa mtoto alimkimbia mama akiwa mjamzito. |
| 10 | *Palasu* | Me | Alizaliwa wakati wazazi wanadharauliana. |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Hivyo basi, kupatikana kwa data hizi uwandani kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji zimedhihirisha kuwa, majina ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo hupewa kutokana na matukio ya vita vilivyotukia katika mazingira wanayoishi. Aidha *Jedwali 1* hapo juu limeonesha kuwa, kuna majina yameonesha yametumika kwa jinsi ya kiume (me) kama vile *Dondo*, *Ndugai*, *Nhizwa* na *Palasu*, *Msuliche na Malugu*. Yapo pia majina ambayo yametumika kwa jinsi ya kike (ke) kwa mfano *Suligwe* na *Ilugu*.

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Vipindi na Misimu**

Majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya vipindi na misimu hutolewa kulingana na vipindi na misimu ya kuzaliwa mtoto. Vipindi au misimu hiyo inajumuisha hali ya hewa, mvua, mavuno, kiangazi na hali ya maisha kwa ujumla. Baadhi ya mifano ya majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya vipindi na misimu imefafanuliwa hapa chini na *Jedwali 2*.

**Jedwali 2: Majina ya asili ya watu yatokanayo na vipindi na misimu**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Mavunde* | Me | (Mawingu) alizaliwa kipindi mawingu yametanda mvua inataka kunyesha. |
| 2 | *Hadikwa* | Ke | (Pandwa) alizaliwa kipindi cha kupanda mazao |
| 3 | *Lubeleje* | Me | Alizaliwa msimu wa kusafisha mashamba. |
| 4 | *Mabuguni* | Me | (Mbelewele) alizaliwa kipindi mahindi yanachanua. |
| 5 | *Mamvula* | Ke | (Mvua) alizaliwa msimu wa mvua inanyesha. |
| 6 | *Manzuwa* | Ke | (kupalilia) alizaliwa wakati wa palizi. |
| 7 | *Haba* | Me | (Chache) alizaliwa msimu wa mvua ndogo. |
| 8 | *Wami* | Ke | (Amia) alizaliwa msimu wa kuamia ndege shambani. |
| 9 | *Manzije* | Ke | (Nzige) alizaliwa kipindi nzige wametokea kuharibu mazao. |
| 10 | *Mazengo* | Me | (Ujenzi) alizaliwa msimu wa ujenzi wa nyumba. |

**Chanzo**: Data ya uwandani

Data zilizowasilishwa katika *Jedwali 2* ambazo zimepatikana kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji zimedhihirisha kuwepo kwa majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yatokanayo na matukio ya vipindi na

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

misimu mbalimbali inayojitokeza katika jamii.

Aidha katika *Jedwali 2* hapo juu linaonesha kuwa, baadhi ya majina hutumika kwa jinsi ya kiume tu kama vile *Mavunde ,Lubeleje,Mabuguni*, Haba na *Mazengo*. Pia kuna baadhi ya majina hutumika kwa jinsi ya kike kama vile *Hadikwa, Mamvula, Manzuwa, Wami na Manzije.*

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Majanga**

Majina ya asili ya watu yanayotokana na matukio ya majanga mbalimbali katika jamii-lugha ya Wagogo majina hutolewa kwa watoto wanaozaliwa wakati wa kipindi cha majanga mbalimbali yanapojitokeza au baada ya muda mfupi kutokea. Majanga hayo yanaweza kuwa ukame, mvua, njaa, baa la nzige na magonjwa yaliyojitokeza. Baadhi ya mifano ya majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya majanga mbalimbali imefafanuliwa hapa chini na *Jedwali 3*.

**Jedwali 3: Majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya majanga**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Ilogo* | Ke | Alizaliwa wakati wa njaa |
| 2 | *Lyagaya* | Ke | Alizaliwa wakati wa shida fulani |
| 3 | *Madeje* | Me | Alizaliwa wakati wa kuamia ndege |
| 4 | *Mandeje* | Ke | Alizaliwa wakati wa kuamia ndege |
| 5 | *Magaya* | Me | Alizaliwa wakati wa shida |
| 6 | *Malogo* | Me | Alizaliwa wakati wa njaa |
| 7 | *Magayo* | Me | Alizaliwa wakati wa shida |
| 8 | *Mamuli* | Me | Alizaliwa radi ilipotokea |
| 9 | *Manhyilu* | Me | Alizaliwa wakati wa shida ya maji |
| 10 | *Mbezwa* | Me/ke | Alizaliwa wazazi wanadharauliana |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Hivyo basi, data zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji zimedhihirisha kuwa majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo hupewa kulingana na matukio yanayotokana na matukio ya majanga yanayotokea katika mazingira yao.

Data za uwandani zinaonesha kuwa, baadhi ya majina hutumika kwa wanaume tu mfano *Midimya* na *Mamuli*. Vilevile yapo majina ambayo hutumika kwa wanawake tu kama *Lyagaya* na *Mgazwa* na mengine hutumika kwa wanaume na wanawake kama vile *Mbezwa.*

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Matukio ya Mungu**

Majina ya asili ya watu yanayotokana na matukio ya Mungu ni majina ambayo huhusisha kifo. Katika jamii-lugha ya Wagogo kifo kinahusishwa na Mungu moja kwa moja. Majina yatokanayo na matukio ya Mungu hutolewa baada ya mtoto kuzaliwa na mzazi mmojawapo kufariki tukio hilo lilihusishwa na Mungu. Kwa hiyo majina hayo yalitolewa kwa jamii-lugha ya Wagogo ili kuweka kumbukumbu ya tukio hilo. Watoto hupewa majina yatokanayo na matukio ya Mungu kama urithi kutoka kwa ndugu wa karibu waliohusishwa na matukio ya kifo. Baadhi ya mifano ya majina hayo imewasilishwa hapa chini na *Jedwali 4*.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

**Jedwali 4: Majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya Mungu**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Kalekwa* | Me/ke | (Kifo) Mzazi au wazazi walifariki mapema (yatima) |
| 2 | *Mchiwa* | Me/ke | (Kifo) Mzazi au wazazi walifariki mapema (yatima) |
| 3 | *Mlekwa* | Me/ke | (Kifo) Mzazi au wazazi walifariki mapema (yatima) |
| 4 | *Ndekwa* | Me/ke | (Kifo) Mzazi au wazazi walifariki mapema (yatima) |
| 5 | *Msolwa* | Me/ke | chukuliwa |
| 6 | *Chilekwa* | Me/ke | Achwa |
| 7 | *Lyadumka* | Me | (Kifo) mzazi au wazazi wote wamefariki |
| 8 | *Chifwiye* | MeKe | (Kifo) mzazi au wazazi wote wawili wamefariki |
| 9 | *Mechiwa* | Me/ke | (Kifo) mzazi au wazazi walifariki mapema |
| 10 | *Suligwe* | Me/ke | Ameachwa yatima |

**Chanzo:** Data za Uwandani

Hivyo basi, majina ya asili ya watu yatokanayo na matukio ya Mungu yamedhihirisha kuwa katika jamii-lugha ya Wagogo watu hupewa majina kutokana na matukio ya Mungu yanayopatikana katika mazingira yao. Aidha, kupatikana kwa data hizi kunadhihirisha kufaa kwa Nadharia na mbinu za mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa zilizotumika kukusanya data. *Jedwali 4* hapo juu linaonesha kuwa, majina mengi yameonesha kutumika kwa jinsi zote.

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Mahali pa Kuzaliwa**

Katika kuendelea kujibu swali la makala haya linalotaka kujua majina ya asili ya watu miongoni mwa majina ya jamii-lugha ya Wagogo, kwa kutumia nadharia ya Uumbaji na mbinu za utafiti imebainika uwepo wa majina ya asili ya watu yanayotokana na mahali pa kuzaliwa. Hata hivyo, majina ya asili ya watu yatokanayo na mahali pa kuzaliwa wakati mwingine huwa hayatokani na mahali pa kuzaliwa bali hutokana na kurithi kutoka kwa wazazi wao au ndugu wa karibu yao. Baadhi ya mifano ya majina ya asili hayo imefafanuliwa hapa chini na *Jedwali 5*.

**Jedwali 5: Majina ya asili ya watu yatokanayo na mahali pa kuzaliwa**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Chigunda* | Ke | Alizaliwa shambani |
| 2 | *Chimehe* | Ke | Alizaliwa sehemu yenye mchwa mwingi |
| 3 | *Chuga* | Me | Alizaliwa sehemu ya kupigia mtama |
| 4 | *Dabaga* | Me | Alizaliwa sehemu yenye tope jingi |
| 5 | *Mabici* | Me | Alizaliwa sehemu yenye miti |
| 6 | *Mahambe* | Me | Alizaliwa wakati wa kuhama |
| 7 | *Mgunda* | Me | Alizaliwa shambani |
| 8 | *Mhyilimo* | Me | Alizaliwa nyuma ya nyumba |
| 9 | *Mihinzo* | Me | Alizaliwa safarini |
| 10 | *Mjendo* | Me | Alizaliwa akiwa matembezini |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Hivyo basi, data zilizowasilishwa katika *Jedwali 5* hapa juu zimedhihirisha uwepo wa majina ya asili ya watu yatokanayo na mahali pa kuzaliwa. Data zimedhihirisha kuwa, watu katika jamii-lugha ya Wagogo hupewa majina kutokana na mahali pa kuzaliwa. Aidha baadhi ya majina yameonesha kutumika kwa wanaume tu kama *Mihinzo, Mjendo* na *Dabaga*.

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Tabia na Matendo ya Watu**

Makala yakiongozwa na Nadharia ya Uumbaji na mbinu za mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

yamebaini kuwa katika jamii-lugha ya Wagogo kuna majina ya asili ya watu yatokanayo na tabia na matendo ya watu. Tabia na matendo ya wazazi au ndugu wa karibu wa familia ama watoto wenyewe ndizo hupelekea watoto kuitwa majina kulingana na tabia na matendo. Baadhi ya mifano ya majina ya asili hayo imefafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 6*.

**Jedwali 6: Majina ya watu yatokanayo na tabia na matendo ya watu**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Chamlomo* | Me | Muongeaji sana |
| 2 | *Chiligati* | Me | Tumo ndani |
| 3 | *Ilumbo* | Me/ke | Shukurani |
| 4 | *Kuhodanga* | Me | Kuharibu |
| 5 | *Majimbi* | Ke | Mnywaji wa pombe |
| 6 | *Makali* | Me | Mkali |
| 7 | *Mapujila* | Me | Mtu mjanja mjanja |
| 8 | *Mdimanghuku* | Me | Mfuga kuku |
| 9 | *Mdimi* | Me | Mchungaji |
| 10 | *Mhatyo/Kaptya* | Me/ke | Mtu mwenye hasira |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Hivyo basi, data katika *Jedwali 6* zimedhihirisha kuwa watu katika jamiilugha ya Wagogo hupewa majina kutokana na tabia na matendo ya watu husika yaliyotendwa na wazazi, ndugu wa karibu au watoto wenyewe katika mazingira wanayoishi. Aidha, data zinaonesha kuwa, baadhi ya majina hutumika kwa wanawake tu kama vile *Majimbi* na majina mengine hutumika kwa wanaume kama vile *Chamlomo*, *Chiligati*, *Mapujila* na *Kuhodanga*. Pia kuna baadhi ya majina hutumika kwa wanawake na wanaume kama vile *Ilumbo*.

### Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Chimbuko la Koo

Kama ilivyo katika jamii nyingine za Kiafrika, katika jamii-lugha ya Wagogo wanaamini kwamba maisha ya mwanadamu ni duara wakiwa na maana kuwa huweza kuanzia katika sehemu moja na kujikuta yamerudi pale yalipoanzia. Katika jamii-lugha ya Wagogo bado majina ya koo yanaendelea kutumiwa kwa kurithishana toka kizazi hadi kizazi. Majina ya koo yanalenga kuwaenzi waanzilishi wa koo husika. Majina yaliyopatikana katika kundi hili tafsiri yake ilihusishwa na ukoo husika. Kwani kulikuwa na miiko fulani ambayo kila koo ilibidi kufuata na miiko yao ilihusisha sana kutokula chakula fulani hasa wanyama na ndege . Kila ukoo ulikuwa na jina lake na miiko yake ambayo mwana ukoo hapaswi kufanya kinyume na miiko hiyo. Hivyo basi, mwana ukoo yeyote ambaye alikuwa akikaidi miiko hiyo waliamini kuwa kuna jambo au tukio lolote baya ambalo linaweza kumpata kama vile kunyonyoka nywele au kung'oka meno yote. Angalia mifano ya majina hayo ya koo kama inavyoonekana katika *Jedwali 7*.

**Jedwali 7: Majina ya asili ya watu yatokanayo na chimbuko la koo**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Mbukwa Lugome* | Me | Hawali nyama ya makongoro ya twiga |
| 2 | *Mbukwa Mubena* | Ke | Hawali nyama ya makongoro ya twiga |
| 3 | *Mbukwa Mahui* | Me | Hawali nyama ya ndege anayeitwa sunha |
| 4 | *Mbukwa Cihui* | Ke | Hawali nyama ya ndege anayeitwa sunha |
| 5 | *Mbukwa Semwali* | Me | Hawali nyama ya swala |
| 6 | *Mbukwa Mnyagatwa* | Ke | Hawali nyama ya utumbo wa mnyama yeyote. |
| 7 | *Mbukwa Mnyambwa* | Me | Hawali nyama ya mbwa |
| 8 | *Mbukwa Muhanga* | Ke | Hawali nyama ya mbwa |
| 9 | *Mbukwa Gawilo* | Me | Hawali nyama ya ndege anayeitwa sunha |

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 10 | *Mbukwa Cituwa* | Ke | Hawali jifu la mnyama yeyote |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Katika *Jedwali 7* data zinadhihirisha kwamba majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yalikuwa yanatolewa kwa wanzilishi kutokana na koo zilizoanzisha jamii-lugha ya Wagogo kama kumbukumbu ya kuendeleza koo zao kwa vizazi vijavyo. Majina hayo mpaka sasa bado yapo katika jamii kama ukumbusho wa kundeleza koo husika ili kutunza mila na desturi ya jamii-lugha ya Wagogo. Makala yamebaini kuwa majina yote yanayotokana na chimbuko la ukoo yanaanza na neno '*Mbukwa'* kama salamu.

Aidha data zimeonesha kuwa, majina ya ukoo yameonesha kutumika kwa wanaume na wanawake kama vile *Mbukwa Lugome*, *Mbukwa Mahui*, *Mbukwa Semwali*, *Mbukwa Mnyambwa* na *Mbukwa Gawilo* ambayo hutumika kwa jinsi ya Kiume (me). Majina mengine hutumika kwa jinsi ya kike (ke) ambayo ni *Mbukwa Mubena*, *Mbukwa Chihui*, *Mbukwa Muhanga*, *Mbukwa Cituwa* na *Mbukwa Mnyagatwa*. Aidha data hizi pia zinadhihirisha kufaa kwa nadharia ya uchunguzi (Uumbaji) na mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa zilizotumika katika utafiti huu.

### Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Majina ya Ujio wa Vitu Vipya

Majina ya asili ya watu yanatokana na majina ya ujio wa vitu vipya. Kwa mujibu wa watoataarifa kupitia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa walieleza kwamba ujio wa vitu vipya katika jamii-lugha ya Wagogo huchangia katika utoaji majina ya watu kwa jamii hiyo. Watoataarifa walidai kuwa, majina ya ujio wa vitu vipya hutolewa kwa watu kutokana na vitu vipya ambavyo vimeingia sasa hapo awali havikuwepo katika jamii. Watoataarifa waliendelea kueleza kwamba lengo la kuwapatia watoto majina hayo ni kuweka kumbukumbu katika jamii yao juu ya ujio wa vitu hivyo. Hebu tuangalie baadhi ya mifano ya majina ya watu yanayotokana na ujio wa vitu vipya katika *Jedwali 8* hapa chini:

**Jedwali 8: Majina ya watu yanayotokana na majina ya ujio wa vitu vipya**

| Na. | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Ndejeulaya* | Me | Ndege ya abiria |
| 2 | *Sajilo* | Me | Mashine |
| 3 | *Mapogo* | Ke | Bangili |
| 4 | *Malolela* | Me | Miwani |
| 5 | *Mkapa* | Me | Raisi wa tatu Tanzania |
| 6 | *Magufuli* | Me | Raisi wa tano Tanzania |
| 7 | *Osama* | Me | Kiongozi wa Alkaida |
| 8 | *Mtuka* | Me | Gari |
| 9 | *Itunhunho* | Me | Pikipiki |
| 10 | *Selela* | Me | Baiskeli |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Majina katika *Jedwali 8* hapo juu yamedhihirisha kuwa watu katika jamii-lugha ya Wagogo hupewa majina kutokana na majina ya ujio wa vitu vipya vinavyojitokeza katika mazingira wanayoishi. Aidha data hapo juu zinaonesha kuwa majina ya ujio wa vitu vipya yaliyokusanywa uwandani kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na nadharia ya Uumbaji, zimeonesha kuwa majina hayo hutolewa kwa wanaume na wanawake kulingana na mazingira husika. Mfano *Mapogo* (Ke) 'bangili' na kwa wanaume ni *Sajilo* (me) 'mashine' na *Malolela* (me) 'miwani.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Majina ya Vitendea Kazi**

Majina yatokanayo na majina ya vitendea kazi ni mojawapo ya vichocheo vya utoaji wa majina katika jamii-lugha ya Wagogo. Majina ya vitendea kazi hutolewa katika jamii-lugha ya Wagogo yakihusisha utengenezaji au utumiaji wa vifaa hivyo wakati wa kuzaliwa mtoto. Makala yalibaini kuwa, utolewaji wa majina hayo hufungamana na muktadha maalum ambao unaweza kuwa wa utengenezaji au utumiaji wake katika vitendea kazi hivyo. Mifano ya majina haya imefafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 9*.

**Jedwali 9: Majina ya watu yatokanayo na majina ya vitendea kazi**

| Na | Jina | Jinsia | Tafsiri ya Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Ndonondo* | Me | Gitaa |
| 2 | *Chibada* | Me | Kibuyu kilichopasuka |
| 3 | *Chihali* | Me | Sahani ya kibuyu |
| 4 | *Izengo* | Me | Mti wa kujengea |
| 5 | *Isili* | Me | Jembe la mkono |
| 6 | *Mandilo* | Me | Mti wa kuchimbia |
| 7 | *Itelejita* | Me | Trecta |
| 8 | *Nghusililo* | Me | Mti wa kukusanyia majani |
| 9 | *Heneko* | Me | ungo |
| 10 | *Isajilo* | Me | mashine |

**Chanzo**: *Data* ya Uwandani

Hivyo basi, data za *Jedwali 9* zimedhibitisha kuwa katika jamii-lugha ya Wagogo kuna majina ya asili ya watu yatokanayo na majina ya vitendea kazi vinavyotumiwa na wanajamii husika. Aidha majina yote yalikusanywa kutoka uwandani kwa kutumia njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji yameonesha kuwa majina yote hutumika na wanaume kwa sababu ya majina ya vitendea kazi vilionesha kutumika au kutengenezwa na wanaume zaidi kuliko wanawake.

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Majina ya Wadudu**

Katika jamii-lugha ya Wagogo kuna baadhi ya majina ya asili ya watu yatokanayo na majina ya wadudu wanaojitokeza katika mazingira yao. Majina ya watu yatokanayo na majina ya wadudu hutolewa kwa wanzilishi baada ya kuzaliwa. Watoataarifa walieleza kuwa majina hayo katika jamii yao hutolewa mpaka sasa kuna baadhi ya watoto wanapewa majina hayo kama majina ya urithi kutoka kwa ndugu zao wa karibu ambao majina yao yalihusishwa na majina ya wadudu. Baadhi ya mifano ya majina yanayotokana na wadudu imefafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 10*.

**Jedwali 10: Majina ya watu yanayotokana na majina ya wadudu**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Mmehe* | Me | mchwa |
| 2 | *Nyawaje* | Me | Washa washa |
| 3 | *Makutupa* | Me | Kunguni |
| 4 | *Chimehe* | Ke | Mchwa |
| 5 | *Nyakongo* | Me | Siafu |
| 6 | *Nyanzije* | Ke | Nzige |
| 7 | Ipalata | Me | Mende |
| 8 | *Nzuguni* | Me | Mbu |
| 9 | *Mahazi* | Me/ke | Nzi |
| 10 | *Madondola* | Me | Manyigu |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Katika sehemu hii, kupatikana kwa majina ya asili ya watu yanayotokana na majina ya wadudu kunatimiza lengo la makala haya linalolenga kukusanya na kuanisha majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo. Aidha, kupatikana kwa data hizi kutoka uwandani kumedhihirisha kufaa kwa nadharia ya uchunguzi (Nadharia ya Uumbaji) na mbinu za utafiti zilizotumika. Kutokana na data zilizowasilishwa hapo juu inadhihirisha kwamba baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo hutokana na majina ya wadudu wanaojitokeza katika mazingira wanayoishi.

**Majina ya Asili ya Watu Yatokanayo na Utani**

Baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo yanatokana na sababu ya utani. Watoataarifa walieleza kuwa, majina ya utani hupatikana kwa wahusika kwa kujiita wao wenyewe, kutaniwa na watu wengine kulingana na tabia zao au kuitwa na jamjj husika kufuatana na tabia ya mhusika, matendo ya mhusika, mwonekano wa muhusika na hata upendeleo wa mhusika fulani katika mambo yake.

Watoataarifa walieleza kwamba, majina ya asili ya watu yanayotokana na utani baadhi yao yanapatikana katika mikusanyiko mbalimbali kama vile ngomani, vilabuni, misibani, harusini na mikusanyiko mingine ya kifamilia. Mhusika wa jina anaweza akajiita jina lolote na la mtu yeyote liwe la mwanaume au la mwanamke kwa kuangalia udhaifu wake kama kumkebehi mtu huyo ama umaarufu wake kama kumsifia mtu huyo. Majina ya utani katika jamii-lugha ya Wagogo mengi huwa ni ya wanaume. Kwa wanawake huwa ni nadra sana mpaka huyo mwanamke afanye kitu cha pekee sana katika jamii. Baadhi ya majina ya asili ya watu yanayotokana na utani imefafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 11*.

**Jedwali 11: Majina ya asili ya watu yatokanayo na utani**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Kupapalima* | Me | Mtu asiye tulia sehemu moja |
| 2 | *Msechenejela* | Me | Mtu anayecheka tu pombe ikiwepo |
| 3 | *Manyusi* | Me | Manyoya ya kuku ya nyuma |
| 4 | *Waiko* | Me | Huna kitu au jambo lolote |
| 5 | *Nzwiya* | Me | Mtu mwenye umbo dogo kama vifaranya vya kuku / bata |
| 6 | *Makutu* | Me | Mtu mwenye masikio makubwa |
| 7 | *Alamutwe* | Me | Mtu mwenye akili sana ama kuwa na kichwa kikubwa |
| 8 | *Kongawadodo* | Me | Danganya watoto |
| 9 | *Majimbi* | Ke | Mnywaji wa pombe |
| 10 | *Mbonelabehi* | Me | Onea karibu |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Data zilizopo hapo juu zinadhihirisha kwamba katika jamii-lugha ya Wagogo kuna majina ya asili ya watu yatokanayo na utani na majina mengi yaliyojitokeza ni ya wanaume. Hivyo basi, data hizi zimedhihirisha kuwa majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo baadhi ya watu hupewa majina kutokana na utani unaoendeshwa katika mazingira wanayoishi.

Aidha katika *Jedwali 11* data zinaonesha kuwa, majina mengi yaliyojitokeza hutumika na wanaume kama vile *Kupapalima*, *Mbedegalo*, *Mkongawadodo na Alamutwe* pia kuna jina moja limejitokeza la mwanamke *Majimbi* ‘mnywaji wa pombe. Data ilikusanywa na mtafiti kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa na aliongozwa na Nadharia ya Uumbaji.

**Majina ya Watu Yatokanayo na Majina ya Wanyama**

Majina ya asili ya watu yatokanayo na majina ya wanyama maana zake zinahusiana na majina ya wanyama. Kundi hili la majina hujumuisha Wanyama wafugwao na wanyama pori ambao

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

wanapatikana katika maeneo husika.

Data zilizowasilishwa katika *Jedwali 12* inabainisha kuwa baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo maana yake hutokana na majina ya wanyama ambao wanapatika kwa wingi katika mazingira wanamoishi. Miongoni mwa majina ya wanyama waliobainishwa katika utafiti huu ni wanyama wa kufugwa na wanyama wa porini. Kupitia njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa imebainika kuwa majina ya asili ya watu yanayotokana na majina ya wanyama mengi ni ya kiume. Wanawake hawakuweza kupatiwa majina yatokanayo na majina ya wanyama kwa sababu katika jamii-lugha ya Wagogo ni jamii ya wawindaji na wafugaji hivyo wanaume ndio hufanya shughuli hiyo ya uwindaji na ufugaji wanawake hawahusishwi katika shughuli hizo. Mifano ya majina yatokanayo na majina ya wanyama inafafanuliwa hapa chini katika *Jedwali 12*.

**Jedwali 12: Majina ya watu yatokanayo na majina ya wanyama**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Chamhene* | Me | Mbuzi |
| 2 | *Ndogowe* | Me | Punda |
| 3 | *Masimba* | Me | Simba |
| 4 | *Mbisi* | Me | Fisi |
| 5 | *Majedengwa* | Me | ngedere |
| 6 | *Nyanholo* | Me | Kondoo |
| 7 | *Mang'ombe* | Me | Ng'ombe |
| 8 | *Ngubi* | Me | Nguruwe |
| 9 | *Fudi* | Me | Panya |
| 10 | *Mbogo* | Me | nyati |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Data zilizowasilishwa zimepatikana kwa mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa na kudhihirisha kwamba baadhi ya majina ya asili ya watu katika jamiilugha ya Wagogo hutumia majina yatokanayo na majina ya wanyama wanaopatikana katika mazingira yao wanaoishi. Majina ya wanyama hao yana maana ambayo inaweza kutofautiana kutoka eneo moja kwenda eneo jingine kulingana na athari ya mnyama huyo katika jamii husika kama Nadharia ya Uumbaji inavyoeleza kuwa, lugha za jamii yakiwepo majina yanasaidia kufahamu utamaduni, historia, mazingira, hali za kiuchumi na kisiasa katika jamii husika.

Majina haya hutolewa kwa watoto wadogo au watu wazima kwa kuitwa wenyewe kulingana na sababu mbalimbali kama vile umbile, upendeleo, matendo au tabia ya mtoto au mtu mwenyewe. Majina haya huakisi utamaduni wa ufugaji na uwindaji. Majina yanayoakisi ufugaji na uwindaji, yanaendelea kupatikana katika jamii-lugha ya Wagogo kwa sababu watu wengi wanaoishi katika mazingira husika ni wafugaji na wawindaji.

### Majina ya Watu Yatokanayo na Hali ya Kipato cha Familia

Haya ni majina ya asili ya watu yaliyotolewa kulingana na hali ya kipato cha familia husika. Majina ya asili ya watu yatokanayo na hali ya kipato cha familia huhusiana na familia kuwa na hali nzuri au hali mbaya ya kipato cha familia. Baadhi ya majina ya asili ya watu yatokanayo na hali ya kipato cha familia yanaoneshwa na *Jedwali 13* hapa chini:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

**Jedwali 13: Majina yawatu yatokanayo hali ya kipato cha familia**

| Na | Jina | Jinsi | Tafsiri kwa Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 1 | *Mapesa* | Me | Pesa |
| 2 | *Mang'ombe* | Me | Ng'ombe nyingi |
| 3 | *Tajili* | Me | Tajiri |
| 4 | *Lyagaya* | Ke | Mateso |
| 5 | *Magayo* | Me | Masumbuko |
| 7 | *Waiko* | Me | Hana kitu |
| 8 | *Ngayo* | Me | Sumbuka |
| 6 | *Lyanini* | Me | Wa nini |
| 9 | *Mtaze* | Me/ke | Saidia |
| 10 | *Mgazwa* | Me | Msumbufu |

**Chanzo**: Data ya Uwandani

Hivyo basi, data zilizopo hapo juu zimedhihirisha kuwa, watu katika jamii-lugha ya Wagogo hupewa majina kutokana na hali ya kipato cha familia husika. Aidha katika *Jedwali 13* data zimeonesha kuwa, majina karibu yote yaliyokusanywa uwandani kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji yameonesha kutumika kwa wanaume tu.

### Majina ya Yatokanayo na Majina ya Urithi

Majina ya urithi ni majina ambayo hupatikana katika familia kwa kurithiwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine. Majina ya urithi hutolewa kutokana na uhusiano uliopo kati ya mtoa jina na yule mwenye jina ambaye jina lake hutumiwa katika utambulisho wa mtoto. Kwa kuwa jina humsadifu mwenye jina hivyo hivyo jina hilo pia huweza kumwathiri mtoto au mtu atakayerithi jina hilo la mwanzilishi. Hivyo basi, katika jamii-lugha ya Wagogo majina ya asili ya watu mengi hutolewa kwa kuzingatia urithi ambapo watoto au watu hurithi majina hayo kutoka kwa ndugu na jamaa zao wa karibu kama vile baba, mama, babu, bibi, mjomba, shangazi na wengineo kwa kutegemea uhusiano walionao. Kwa kuzingatia kigezo cha urithi mtoto aliweza kupewa jina la kurithi kutoka kwa mtu aliye hai au ambaye tayari alishafariki. Kwa mujibu wa watoataarifa waliofikiwa na mtafiti kwa njia ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa kwa kuongozwa na Nadharia ya Uumbaji walieleza kuwa, majina ya urithi hutolewa kwa ajili ya kutunza kumbukumbu, kuweka utambulisho, kutaka kuyaendeleza majina ya waanzilishi hao katika jamii na kuzidisha upendo, ushirikiano na mshikamano baina ya wanafamilia. Watoataarifa waliendelea kueleza kuwa, majina ya kurithi hayajibainishi kiupekee kwani majina ya urithi hupatikana katika vigezo vingine vinavyozingatiwa katika utoaji majina ya asili katika jamiilugha ya Wagogo. Baadhi ya majina yanayotokana na urithi ni pamoja na *Kuhodanga*, *Mwendwa*, *Ilumbo*, *Chipegwa*, *Udoba*, *Mnyanyi*, *Suligwe*, *Chilongani*, *Mabichi*, *Chiligati*, *Ichenda*, *Mapesa*, *Mapugila*, *Chiuyo*, *Lyagaya*, *Magayo*, *Malugu*, *Matonya*, *Mazengo*, *Malejehe*, *Matika*, *Mbelege*, *Manzige*, *Chamlomo*, *Lomolomo*, *Mtemi*, *Isajilo* na mengineyo.

## HITIMISHO

Katika kujibu swali la makala haya lililotaka kujua majina ya asili ya watu yanayotumika katika jamii-lugha ya Wagogo. Makala kupitia mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa yakiongozwa na nadharia ya Uumbaji ya Sapir-Whorf (1958), makala yamebaini kuwepo kwa makundi kumi (10) ya majina yenye tasfsiri mbalimbali. Makundi hayo ni pamoja na majina yanayotokana na matukio, mahali pa kuzaliwa, tabia na matendo ya watu, chimbuko la ukoo, majina ya ujio wa vitu vipya na majina yatokanayo na wadudu. Vile vile kuna majina yanayotokana na utani, majina ya wanyama, kipato cha familia na majina ya urithi.

## MAPENDEKEZO

Kutokana na data iliyowasilishwa kuhusu majina ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo, makala haya yanapendekeza mbinu mbalimbali za kutumia ili kuendeleza matumizi ya majina ya asili ya watu katika jamii-lugha ya Wagogo.

Kwanza, ni kutoa elimu kwa njia mbalimbali kwa jamii-lugha husika juu ya umuhimu wa majina ya asili, maana za majina hayo, matumizi yake ili waweze kuyatumia katika miktadha mbalimbali ili yasipotee.

Pili, majina ya asili hayapaswi kupuuzwa na kubezwa kwani majina hayo yamebeba utamaduni wa jamii husika. Hivyo, kupuuzwa na kubezwa kwa majina haya ni sawa na kupuuza utamaduni wa jamii hiyo ambapo utamaduni ndio unabeba kila kitu cha jamii husika. Matokeo yake ni kusababisha kupoteza utambulisho kwa vizazi vijavyo.

Tatu, kutoa elimu hasa kwa vijana ili kuongeza uelewa na kuchochea utambuzi wa umuhimu wa kutumia majina ya asili ili kujifunza, kuenzi na kudumisha utamaduni wao ikiwa ni pamoja na kuwafanya wajivunie na kuona fahari kuitwa kwa majina yao ya asili tofauti na ilivyo sasa ambapo wanapenda kutumia majina ya kigeni.

Mwisho kwa kuwa majina ya asili ya watu kwa ujumla yanakabiliwa na tatizo la kukaribia kupotea kabisa, majina haya yanahitaji kulindwa kwa kuwekewa mikakati maalumu na jamii-lugha husika kwa kuyalinda, kuyahifadhi, kuyatunza, kuyaenzi na kuyaendeleza kwa faida ya kizazi kijacho na taifa kwa ujumla.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Jina -** Jina ni neno linalotaja mtu, kitu au mahali (TUKI, 2004). Pia jina huweza kumtofautisha mtu mmoja na mwingine, kitu kimoja na kingine n ahata sehemu moja na nyingine. Jina pekee ndilo huweza kutambulisha mtu, kitu n ahata mahali fulani.

**Majina ya Asili -** Majina ya asili ni majina ambayo, chimbuko, historia na maana hutokana na taratibu za tamaduni za jamii husika (Nyangawa, 2013). Majina ya asili katika jamii nyingi hutokana na lughamama ambazo hutumika katika kuwasiliana na pia maana za majina hayo hujulikana na jamii husika.

**Jamii-lugha -** Jamii-lugha ni watumiaji wa lugha wanaoishi katika eneo moja ambao hubainishwa kaw mahusiano yao ya kuendelea kutumia aina fulani ya lugha, tofauti na watumiaji wengine wa lugha hiyo (Msanjila &Wenzake, 2009).

**Wagogo -** Wagogo ni kabila kubwa nchini Tanzania, wanaishi katika mkoa wa Dodoma. Lugha yao ni Cigogo (kwa Kiswahili hutumika Kigogo). Wagogo hutambuliwa kwa kutoga masikio, ndonye kwenye paji la uso na kutoa jino moja (Mnyampala, 1954).

## MAREJELEO


Anusa, H. J. (2016). *Maana za Majina ya Watu Katika Jamii ya Wayao*. Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Dawling, T. (2004). “Uquidisizwe” The Finisher of Nation, Naming and Taking a bout HIV/AIDS and African Languages. ht tp:/www. African voice.co.za/research. Htm.

Koigi. J. (2008). Literary Scene: What is in name. *Daily Nation.* Nairobi Medi Group, uk 37.

Gray, T. M. (1999). What’s in a name? Some reflection on the Socialogy Annonymity. http//web.ed/gt marx/a non.html.

Kalkanova, T. (1999). Sociology of Proper Names in Sophia since 1970. *International Journal of Sociology of Language*, 135, 83-98.

Matsimela, A. M. (1997). *Sefulediso*. Republic of South Africa: Creda Press.

Mbiti, S. (1990). *African Religion and Philosoph*. USA: Heinemann Educational Books inc.

Mnyampala, M. E (1954). *Historia, Mila na Desturi za Wagogo*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.


This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1303

Musere, J. (2010). *African Person Names Derived from African Pro*. llE line aArhicle. Com/2expert=Jonathan Musere.

Nyangaywa, M. (2013). *Uchunguzi wa Kisemantiki na Taratibu za Utoaji wa Majina* ya *Kijita*. Tasnifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ota, O. (2002). *Edo Person Names and World View*. New Perspective in Edoed Studies; Nigeria.

Rey, A. (1995). *Essay on Teminology*. Amsterdam, John Benjamin Publishing Company.

Rugemalira, J. M. (2005). *A Grammer of Runyambo*. Dar es Salaam: Language of Tanzania Project. University of Dar es Salaam.

Sapir, E. (1921). *Language*. New York: Harcourt Brace.

Sapir, E. (1958). *Language*. New York: Harcourt, Brace & Co.

Tegisi, N. M. (2019). *Uchunguzi wa Kisemantiki wa Majina ya Asili Katika Ginantuzu*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Whorf, B. L. (1958). *Language Thought and Reatily*: *Selected Writings.* Cambridge, Technology Press of Massachusetts Institute of Technology.

Zacharia, M. (2020). *Matumizi ya Majina ya Kiswahili Jijini Dar es Salaam, Nchini Tanzania*: *Uchunguzi Kifani wa Majina ya Watu*: Tasnifu M. A Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.